# Sera ya Kulinda Mtoto

**Namba ya Sera:** 320
**Tarehe rasmi ya Kuanza:** Juni 2020
**Tarehe Itakayofuata ya Mapitio ya Pili:** Mai 2022
**Mmiliki wa Sera:** Afisa Mkuu wa Maadili na Matekelezo

*Sera hii inatangulia sera zote za awali zinazohusu ulinzi wa watoto.*

## Lengo

Pact inaamini ya kwamba maslahi ya mtoto ni muhimu zaidi. Sera hii inaangalia uhakika wa usalama kwa watoto wote wanapojumuishwa katika miradi inayoendeshwa moja kwa moja au vinginevyo (kupitia wakandarasi wadogo) na Pact. Tumejitolea kuzuia madhara yeyote kwa watoto na kuwajibika mara moja na kwa njia inayofaa kuhusu madai yeyote ya unyanyasaji.

## Matumizi

Sera hii inatumika kwa wafanyikazi wote, washauri, wakandarasi huru, wakala na wanaojitolea wote kwa ujumla ("Wafanyikazi"), na wageni ("Wageni") ambao hufanya kazi kwa au kutembelea Pact na miradi ya wakandarasi wadogo wa Pact inayohusu watoto.

## Miongozo ya Jumla

### *Tabia Zinazopigwa Marufuku*

Tabia zilizopigwa marufuku wakati wa kushughulika na mtoto zinajumuisha, lakini sio hizi pekee:

- Kuwapa watoto nidhamu au adhabu za kimwili.
- Kushiriki katika shughuli za kingono na watoto bila kujali umri wa idhini ya kujihusisha na ngono katika nchi husika, au umri unaodhaniwa wa mtoto.
- Kuwafanyia watoto mambo yao binafsi ambayo wangeweza kufanya wao wenyewe.
- Kuwaalika watoto nyumbani kwako, isipokuwa kama msimamizi wako amekubali kuwa ni muhimu kwa usalama wa mtoto.
- Kulala kitanda kimoja au chumba kimoja na mtoto. Ikiwa italazimika kulala chumba kimoja, hakikisha kuwa kuna mtu mzima mwingine au umepata ruhusa kutoka kwa msimamizi wako.
- Kuwa katika uhusiano na watoto ambao kwa njia yoyote inaweza kuonekana kuwa isiyofaa, ni ya dhuluma au ya unyanyasaji.
- Kuwapatia watoto hela kama zawadi au kubadilishana mawasiliano binafsi na mtoto.
- Kufanya mambo namna ambayo kwa kusudi au sio kusudi kuwaaibisha, kuwafedhehesha au kuwashusha hadhi/thamani watoto, au kuwanyanyasa kimawazo.
- Kuwabagua au kuonesha utofauti unapo washughulikia kwa lengo la kuwatenga watoto.
- Kutumia lugha au kuonyesha watoto tabia isiyofaa, ya kikatili au yenye kuchochea hisia za kingono.
- Kuajiri watoto katika kazi za nyumbani au kazi nyingine zinazokiuka sheria za kazi za nchi, haifai kulingana na umri wao au katika maendeleo yao ya ukuaji au kuwaweka katika hatari kubwa ya kuumia.

- Kutumia kompyuta yoyote, simu za mkononi, kamera za video, mitandao ya kijamii au teknolojia nyingine kunyanyasa watoto.
- Kuangalia picha za watoto za unyanyasaji wa kingono kupitia chombo chochote.

***Miongozo ya Mitandao ya Kijamii na Upigaji Picha***

Mawasiliano yote ya ndani na ya nje kuhusu watoto ni lazima yazingatie miongozo hii:

- Kuhakikisha kuwa taswira za watoto zilizochukuliwa (k.m. picha, video) ni sahihi na zina heshimu faragha na utu wa watoto, ikifuata miongozo ya Pact ya mawasiliano ya kimaadili, inayopatikana katika ukurasa wa 6 wa Mwongozo wa Chapa Sanifu. Watoto lazima wawe wamevaa nguo zinazofaa katika picha. Mikao inayoashiria hisia za kingono hairuhusiwi.
- Kabla ya kupiga picha, pata idhini ya maneno kutoka kwa watoto na idhini ya kujulishwa kutoka kwa walezi wao ukitumia Fomu ya Pact ya Kutoa Picha. Watoto na walezi wanapaswa kuelezwa jinsi picha zao zitakavyo tumika.
- Utumiaji wa picha za watoto iwe tu kwa madhumuni ya kitaaluma, heshima, kuelimisha umma, kuchangisha fedha, kupata umaarufu na kwa matumizi ya mradi.
- Hakikisha kuwa picha yoyote au kumbukumbu ya historia ya mtoto haiwaweki katika hatari ya ziada au urahisi wa kudhuriwa na aina yoyote ya unyanyasaji.
- Heshimu faragha za taarifa zote zinazowahusu watoto. Zingatia sheria za ulinzi wa taarifa na toa taarifa hizo endapo tu kuna umuhimu wa kujua mambo ya msingi, huku ukizingatia haki yao ya faragha.

***Kuripoti ya Lazima***

Wafanyikazi na wageni wanahitajika kuripoti shauku au madai ya unyanyasaji wa mtoto au dhuluma, au kutofuata sheria na sera hii, ndani ya saa 24 kwa kuarifu Afisa Mkuu wa Ufuatiliaji Sheria na Maadili au kwa kutuma ripoti kwa Mfumo wa Sehemu ya Kuripoti Maadili. Wafanyikazi wa Pact na wageni wanapaswa pia kuripoti madai yeyote ya kihistoria yanayohusika kwa uwekaji salama katika miradi yote vya Pact. Miongozo ya kuripoti na kuchunguza tuhuma au madai ya unyanyasaji wa mtoto au dhuluma zimeorodheshwa katika Miongozo ya Pact ya Kulinda Kuripoti Uchunguzi wa Mtoto.

Tafadhali tambua kwamba Sehemu ya Maadili si huduma ya dharura na inapaswa kutumiwa pale tu baada ya mtoto (au watoto) kuokolewa kutoka hatarini kwa wakati huo. Kama mtoto amekaribia hatari, mfanyikazi anapaswa kuarifu mara moja Mkurugenzi wa Nchi (CD) husika, kama inawezekana, ili waweze kuwasiliana na kitengo cha kusimamia sheria kwa dharura au mamlaka nyingine sahihi au serikali za mitaa. Ni baada ya hapo tu mfanyikazi anatakiwa kuripoti madai ya matukio kwa Afisa Mkuu wa Maadili na Matekelezo au kwa kujaza ripoti kupitia Sehemu ya Maadili.

## Utekelezaji

***Muundo wa Mradi***

Wafanyikazi wa Pact wanao wajibu wa kuunda, kupanga bei, kugharamia na kutekeleza miradi, moja kwa moja au kupitia wakandarasi wadogo, wanao wajibu wa kulinda watoto wanaohusika na miradi hayo. Wafanyikazi wa Pact katika mradi na maendeleo ya biashara wana wajibu wa kuunganisha Mpango wa Pact wa Matekelezo na Ulinzi wa Mtoto, uliofupishwa katika Orodha ya Ulinzi wa Mtoto, ndani ya mradi mzima na mapendekezo ya mkandarasi mdogo. Mpango wa Ufuatiliaji Sheria na Kulinda Mtoto unajumuisha hati zifuatazo:

- Orodha ya Kulinda Mtoto

- Itifaki ya Tabia ya Kulinda Mtoto / Mtandao Wa kijamii na Miongozo ya Picha
- Miongozo ya Uchunguzi na Kuripoti Kulinda Mtoto
- Kielezo cha Wakandarasi wadogo cha Itifaki ya Tabia ya Kulinda Mtoto (Kifaransa, Kihispania, Kiswahili)
- Barua na Fomu ya Matekelezo ya Mkandarasi Mdogo ya Kulinda Mtoto (Kiingereza, Kifaransa, Kihispania, Kiswahili)
- Mabango Kuonesha Tabia Kiitifaki katika Ofisi za Nchi (katika lugha 17)
- Mtandao Wakijamii na Miongozo ya Mabango ya Picha za Ofisi za Nchi (katika lugha 17)

***Ofisi za Nchi***
Wakurugenzi wa Nchi (CD) ni lazima wahakikishe kwamba hali zote za Mpango wa Kulinda Mtoto zimetekelezwa katika ofisi yao na ndani ya miradi ya nchi. Wakurugenzi wa Nchi wanaweza kugawa majukumu, kama inavyofaa, kwa washirika wa timu yao, Mkuu wa Chama, au Meneja mwingine mkuu anayewajibika, lakini Mkurugenzi Mkuu anabaki na jukumu la mwisho la kuhakikisha watoto wako salama kulingana na viwango maalum vya Pact.

Ofisi zote za Pact zinahitajika kuonesha mabango ya Pact ya Kulinda Mtoto (ikionesha Itifaki ya Tabia ya Pact na Miongozo ya Mitandao ya Kijamii na Picha) inayojitokeza vyema kwa wafanyikazi na wageni wote ili waweze kuiona kwa urahisi.

Mkurugenzi Mkuu anao wajibu wa kutambua rasilimali zote za dharura katika nchi yao ili kuripoti tuhuma ya ukiukwaji wa kulinda mtoto. Rasilimali hizi zinapaswa kuwasiliwa mara moja endapo mtoto au watoto wamepatwa na hatari. Miongozo ya Pact ya Uchunguzi na Kuripoti ina amuru kwamba ripoti inapaswa kujazwa kulingana na Mfumo wa Pact wa Sehemu ya Kuripoti Maadili ndani ya saa 24.

***Kuajiri na Kukagua***
Afisa Rasilimali Watu wana wajibu wa kuhakikisha kwamba wakati wa mchakato wa usaili, waombaji wa nafasi zinazohusu na mwingiliano na watoto wanaulizwa kuhusu kazi zao za awali na watoto na kupeana angalau wadhamini wawili (2) kutoka kwa kazi za awali zilizo na uzoefu na watoto. Wakati inakubalika na sheria ya maeneo hayo, waombaji wataulizwa wapeana idhini ya maandishi kuhusu hati zao za makosa ya jinai au taarifa ya polisi kuhusu mienendo yao zamani ili kufahamu kuhusu makosa yeyote yanayohusiana na unyanyasaji wa mtoto au unyanyasaji wa kijinsia. Pact haita ajiri mtu yeyote kwa kufahamu ya kwamba mtu huyo alikuwa na historia ya awali ya unyanyasaji wa mtoto na/au unyanyasaji wa kijinsia na itasitisha ajiri ikitambua historia kama hiyo.

Afisa wa Rasilimali Watu watahakikisha kwamba wafanyikazi wote wa Pact watakiri kupokea na kuelewa Sera ya Kulinda Mtoto na Mpango wa Matekelezo wa Sheria wa Pact wakati wanapo ajiriwa. Wafanyikazi wote wanahitajika kukamilisha kozi ya Mafunzo ya Kulinda Mtoto inayofanyika mtandaoni. Wafanyikazi wanao fanya kazi moja kwa moja na watoto wanahitajika kufanya tena upya na kupata tena cheti cha mafunzo kila mwaka.

***Uchunguzi na Ufuatiliaji***
Ofisi ya Maadili & Matekelezo ina majukumu ya kuhakikisha kwamba madai ya dhuluma au unyanyasaji wa mtoto yana chunguzwa kulingana na Miongozo ya Uchunguzi na Kuripoti Kulinda Mtoto. Katika uchunguzi wote, wafanyikazi wa Pact na wageni wanahitajika kuchangia na kushirikiana katika uchunguzi. Hadi pale itakapo hitajika kivingine, habari zote ni sharti zihifadhiwe kwa usiri kuhusu mwathiriwa/wa athiriwa shukiwa na mhalifu (wahalifu)shukiwa.

Afisa wa Ufuatiliaji Sheria na Mkuu wa Maadili wa Pact na wachunguzi wao wana jukumu la kutekeleza uchunguzi wa ripoti za Kulinda Mtoto. Afisa Mkuu wa Maadili na Matekelezo ni lazima aripoti muhtasari wa data ya matukio kwa Timu ya Wasimamizi Wakuu wa Pact (SMT) na kwa Baraza la Wakurugenzi kila baada ya miezi minne. Afisa Mkuu wa Maadili na Matekelezo aripoti mara moja kesi zote za kipekee kwa SMT na kwa Baraza la Wakurugenzi kama itakavyo hitajika.

Afisa Maadili na Matekelezo pia anao wajibu wa kufuatilia kwamba Sera ya Matekelezo na Kulinda Mtoto na Mpango wa Matekelezo zinazingatiwa.

## Utekelezaji

Ukiukwaji wa Sera ya Kulinda Mtoto na Mpango wa Matekelezo ni sababu tosha za kupeana nidhamu ikijumuisha kufutwa ajira au mkataba kusitishwa. Mshtakiwa anayedaiwa kumnyanyasa mtoto anaweza kusimamishwa katika nafasi yake (kwa malipo) wakati wa uchunguzi wa madai hayo. Mfanyikazi aliye dhibitishwa kwamba amenyanyasa mtoto atafutwa kazi kutoka kwa Pact na hataweza tena kupewa ajira. Wakati tukio la madai limethibitishwa kuwa uwongo au lakutungiwa, hatua mwafaka zitachukuliwa kufuatiliwa mtu aliye shtakiwa, mtoto na mtu aliye peana mashtaka hayo. Mfanyikazi yeyote anaye peana mashataka ya nia mbaya au ya uwongo atapewa nidhamu, hadi kufutwa ajira.